*Jwe la Kiroho la Kujengea 12*

# KWA HIYO VAENI SILAHA ZOTE ZA MUNGU.

***(Waefeso 6:10-20) Kwa sababu hiyo vaeni silaha zote za Mungu mpate kuweza kushindana siku uovu na mkisha kutimiza yote kusimama.***

Sasa je unajuwa tumekuwa na vita baada ya vita na matetesi ya vita? Na kama dunia itaendelea kuwepo tutakuwa na hayo mengi zaidi lakini Je unatambuwa kwamba kuna nguvu halisi mbili katika Dunia yote? Pamoja na tofauti zetu zote kati ya taifa na taifa na tofauti kati ya mtu na mtu na kila kitu vyote hivyo vinaingia katika nguvu mbili, kwa hiyo ni nguvu mbili tu na kuna falme mbili tu nguvu mbili na falme mbili, nyingine zilizobaki ni vitu vidogo vodogo ambavyo vimeunganishwa na nguvu hizo mbili. Na nguvu hizo ni nguvu za Mungu na nguvu za shetani. Kila vita kila kutokuelewana, chochote kile kinachokuja katikati vinatawaliwa na nguvu za Mungu au ni nguvu za shetani kwa sababu hizo ndizo nguvu pekee mbili ambazo zipo. Na hiyo ni nguvu ya uzima na nguvu ya mauti.
Sasa hizo ndizo nguvu mbili peke mbili.

Shetani nguvu zake alizonazo ni nguvu za Mungu zilizopotoshwa . Siyo nguvu halisi ni nguvu zilizopotoshwa za Mungu. Vyovyote vile shetani alivyonavyo. Kifo ni uhai tu au ni uzima tu uliopotoshwa. Uongo ni ukweli ambao umepotoshwa na hapa tulipoleo tukiwa tumekaa hapa moja ya hizi nguvu zitaenda kututawala sisi. Kwa hiyo na tutupe nje nguvu ile moja uovu. Na tuchukuwe nafasi yetu kama nyota za Mbinguni na sasa Jeshi kitu cha kwanza linajiandaa kwa vita. Kwanza unatakiwa kuwa na uchaguzi wa baadhi ya Askari wanapaswa kuvalishwa kwa ajili ya mapambano inabidi wafundishwa namna ya kupigana.

Na nina amini vita kuu ambayo imewahi kupigana iko tayari sasa kuanza. Ninaamini Mungu amekuwa akichaguwa Askari wake, ninaamini alikuwa anawavalisha wao na kuwafundisha wao na kwamba vita ya sasa viko tayari kupigana, vinandaliwa kuanza.

Vita ile kuu ya kwanza ambayo iliwahi kupigana ilianza mbinguni wakati mikaeli na Malaika zake walipopigana dhidi ya Lusiferi na Malaika zake. Ilianzia hapo vita vya kwanza vilianzia mbinguni. Kwa hiyo dhambi haikuanza duniani, ilianza mbinguni. **(Ezekiel 28:11-17),**
**(Isaya 14:12-15).**

Na baada ya hapo vita hiyo ilishuka kutoka mbinguni, walitupa watoke mbinguni kuja duniani na ikawaangukia wanadamu hapo sasa halafu iliangukia wanadamu halafu vita kutoka kwa malaika ikawa ni vita ya wanadamu. Na shetani alikuja kuharibu uumbaji wa Mungu ile Mungu alichoumba kwaajili yake mwenyewe, kile alichokuwa nacho. Shetani alikuja kuharibu hicho na hilo lilikuwa ndilo lengo lake ni kuharibu hicho kwa hiyo vilianza hapa duniani vikaanza ndani yetu na vimekuwa vikiendelea tangu wakati huo. ***(Warumi 7:12-25) (Wagalatia 5:17).***

***(Waefeso 6:10-20)** "Hatimaye, mzidi kuwa hodari katika bwana na katika uweza wa nguvu zake. Vaeni silaha zote za Mungu mpate kuweza kuzipinga hila za shetani kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama…..Siyo kupiga risasi na kukata kwa visu unaona hilo silo hilo" ……… bali ni juu ya falme na mamlaka juu ya wakuu wa giza hili juu ya majeshi wa pepo wabaya katika ulimwengu wa Roho,…"*

"Watawala wa giza" nani anatawala hii dunia? Ni shetani hakika ni nani anayeyafanya haya mambo yote yanayoendelea, haya mambo yote ambayo siyo ya ki Mungu yanayoendelea kila mahali hapa na hizi serikali nakadhalika. Yote haya ni shetani Biblia imesema hivyo shetani ndiye anayetawala Amerika, shetani ndiye anayetawala Ujerumani, shetani anatawala tawala zote za dunia kila ufalme uliowahi kuwepo na utakao kuwa mpaka Mungu atakapoweka Ufalme wake, Falme zote zinatawaliwa na shetani ***(Matayo 4:8-11)*** Simanishi kwamba kila aliyeko serikalini ni shetani sasa  kuna watu wa Mungu katika ofisi za serikali.

"Uovu wa kiroho katika sehemu za juu" Sasa nisikilizeni ninyi askari wote "chukuweni silaha zote (siyo sehemu tu) silaha zote za Mungu ili  muweze kusimama katika siku ya uovu. Hiyo ndo siku tunayoishi ndani yake.

"Mkiwa mmefanya yote kusimama "kusimama… Ameen unapata hilo unapokuwa umefanya yote uwezayo kufanya kusimama hapo sasa simama usisogee " Kwahiyo simameni mkiwa mmefungwa viunoni mwenu….."

Sikiliza hapa angalia hili ni nini? "Viuno vyenu" hiyo ni sehemu yako ya katikati hapa "ifungiwe na ukweli"  Kweli ni nini? Neno la Mungu ni kweli ***(Yohana 17:17)*** hiyo ni sahihi neno la Mungu ni kweli " Neno la Mungu ni kweli vema "Mkiwa na ***Ngao ya Imani***" Hiyo ni " fanya lililo sahihi" uwe na neno la Mungu ndani yako ukifanya yaliyo sahihi ngao ya imani kifuani"  Na miguuni mwenu muwe mmefungiwa utayari wa kuhubiri injili ya amani" Nenda mahali popote wakati wowote miguu yenu ikiwa imefungiwa utayari juu ya yote haya chukuwa ngao ya imani. Hiyo ndiyo pekee iwezayo kuishinda mishale hicho ndicho kitu kimoja kinachoweza kuizima mishale unaona "Ngao ya imani"

"Ambapo utaweza kuizima mishale yote ya moto ya Yule muovu na uchukue chepeo ya uokovu" Nia iko hapa katika kichwa inafunika kichwa. "….na upanga wa Roho ambao ni neno la Mungu." Hi  chepeo inafanya kazi kwa namna gani? Na inalinda je hi chepeo imetengenezwa na nini? Imetengenezwa na shaba. Shaba ni ngumu sana kuliko chuma hii inawekwa kitu cha kichwani wokovu, maarifa ya kujuwa hili " Uponyaji wangu unakuja kutoka kwa Mungu uwokovu wangu unapatikana kutoka kwa Mungu, uzoefu wangu unalingana na neno lake, siyo mawazo ya makanisa ni neno . Ameni! Huko hapo umefunikwa ukiwa na kitu cha kukulinda chepeo ya uwokovu kufunguliwa chukuwa hilo halafu endelea kutembea mbele  oh! Sasa hicho ndicho tunachopaswa kufanya.  Jeshi la shetani…. Sasa angalia jeshi la shetani linaleta magonjwa hicho ndicho shetani alicho yeye ni mharibifu Shetani , ufalme wote wa shetani ni magonjwa kufa, na huzuni na vitu vya kuchanganya akili na wasiwasi vyote viko kwa shetani. Mungu ni uzima, imani,furaha, amani, vyote hapa. Sasa hizo ndizo nguvu mbili ambazo zinakuja pamoja sasahivi  zinapigana, zinapigana sasa hivi katika jingo hilo tulilopo zinapigana siku kwa siku na wewe kila nguvu kwa msaada wa Mungu unalindwa  kwa injili ambalo ni neno la kweli linalokuzunguka kiunoni kwako. ***(Waefeso 1:13-14).*** Utukufu! Wahubiri, hivyo ndivyo ilivyo

ngao ya imani na upanga ukivipepea mkononi mwako " shetani ninakuja kukutana na wewe" Wewe unakuja kwa jina la vyama na unakuja kukutana na mimi kwa jina la hiki na kile au chochote. Lakini mimi ninakuja kukabiliana na wewe kwa Jina la Bwana Mungu wa Iziraeli ninakuja kukutana na wewe achilia! "Hata kifo chenyewe hakiwezi kusimama pale toboa tundu kupitia hicho hiyo ni sahihi .

Jeshi la shetani linaleta magonjwa na Jeshi la Mungu limeamriwa kuyatoa magonjwa yatoke. Tuko hapo kila mara shetani anapokutupia chochote kati ya hayo , Jeshi la Mungu kazi yake ni kuyatoa nje Ameni. Kuyatoa nje! Hiyo ndiyo mbinu ambayo Mungu anaitumia shetani anatumia jeshi la uharibifu kufanya kutokuliamini neno la Mungu kufanya neno la Mungu lisiaminike na kuweko ufalme ulio mzuri zaidi kuliko Mikaeli alio kuwa nao, Mungu alimtupa chini utaratibu wa Mungu kitowe nje kilicho kiovu tupa chini hoja, tupa chini ushirikina, tupa chini hofu, tupa chini magonjwa, tupa chini dhambi Ameni. Wewe uko juu ya haya umefufuka ndani ya Kristo Yesu ukiwa umeketi katika ulimwengu wa Roho na kila pepo likiwa chini ya miguu yako kama akijaribu kuamsha kichwa chake pale ni nini unajuwa wewe umekufa uhai wako umefichwa ***(Wakolosai 3:1-4)*** Ni nini maana ya kufa umekufa katika hisi zako , umekufa katika ufahamu wako , Ufahamu wako wa kibinadamu umesema ndiyo nawazia umesema umekufa katika hoja zako , umekufa katika mambo hayo yote na umezikwa kwa Jina la Yesu Kristo , Umefufuka pamoja naye ***(Rumi 6:1-15)*** Na popote pale alipo wewe upo pia .

Kuna tokea nini wakati mmoja wa hawa wenye shaka atakapofika mbinguni? Mungu alimpiga teke atoke . Na Yeye alisemaje kwa Askari wake ambao wamefufuliwa katika Kristo " Wakati shetani akija mbele yako mpige teke atoke mtupe nje" Wakati Yesu alipokuwa anafundisha Jeshi lake alipokuwa anawaagiza waende mpaka mwisho wa dunia aliwaambia nendeni ulimwenguni kote hubirini injili kwa kila kiumbe ***(Marko 16:15-18)*** . [1]

Silaha zote za Mkristo kwa hakika ni vitu visivyoonekana (supernatural) . Hakuna chochote kilicho cha asili kama unaweza kumthibitisha Mungu basi itamaanisha hamna haja ya kuwa na imani lakini Yeye anayemjia Mungu lazima amini kwamba yeye yupo ***(Waebrania 11:6)*** Ni kwa imani silaha zote za Mkristo ni imani Mkristo anangalia mambo asiyo yaona
***(2Wakorintho 4:18)*** Sasa hebu tuchukuwe silaha zote za ukristo kama kweli ni vitu visivyo onekana (Supernatural) upendo, furaha, thamani, amani, imani, uvumilivu, upole, utu wema subira. Kila kitu ni kitu kisichoonekana (Super natural) upendo? " Nenda pale chini ni duka la dawa na uninulie mimi robo ya upendo nina uhitaji" Unaona huwezi ukafanya hilo ninunulie amani yenye thamani ya dola moja huwezi ukafanya jambo hilo unaona?Kila kitu ni visivyonekana silaha zote za Mungu ni vitu visivyoonekana. Kanisa lake ni vitu visivyoonekana haliko kwenye vyama vya kidhehebu ni mwili usionekana ambao wanaume na wanawake wanazaliwa katika hilo kwa Roho Mtakatifu na ni njia rahisi hivyo. ***(1 Wakorintho 12:13)***. [2]

Uzima, Imani upendo, furaha, amani, uvumilivu, upole, utu wema, subira, sayansi haiwezi ikagusa haya na hivyo ndivyo vitu halisi peke vitu vilivyopo vinavyodumu. Silaha zote za Mkristo zinaangalia yale yasiyoonekana lakini zile hisi haziwezi kutangaza mambo haya lakini yako pale hiyo ndiyo sababu inachukuwa imani kuamini hilo na inatoa ndani yako kile ambacho imani imetangaza kwamba kiko pale inakileta pale inakileta kwako. Uponyaji wa kiungu na mengineyo hawawezi kuthibitisha kitu gani kinaponya kiungu lakini wanajuwa kwamba kuna

uponyaji wa kiungu hawawezi kuthibitisha kile kinachotuokoa na dhambi, lakini wanajuwa watu ambao wameokolewa na dhambi kwahiyo haiwezi kuthibitisha kisayansi lakini iko kisayansi katika mwonekano wa njia ya Mungu. [3]

Iangalie hiyo kwa macho yako, unaona kwa moyo wako, unaangalia kitu chochote unasema "sikioni hicho" unamanisha hukielewi hicho [4].

Mkristo siku zote anaangalia mambo ambayo hayaoni kwa sababu anaangalia ahadi. [5].

Tunaangalia vitu ambavyo hatuwezi kuviona kwa macho yetu ya kawaida. [6].

Marafiki wa Kristo vaeni silaha zote za Mungu, usisimame pale nyuma ukiwa na mawazo ya kanuni Fulani au kitu Fulani ambacho unasimama nacho. Vaa silaha zote za Mungu unapoenda kupigana na adui. Kama Bwana wetu alivyofanya. Alionyesha vile ambavyo Mkristo mdhaifu sana anavoweza kumshinda shetani kwakutumia nguvu, Yeye alikuwa na nguvu, angeweza kumpiga shetani kwa vyovyote vile ambavyo angetaka lakini hakuitumia hiyo. Alililichukuwa tu neno na akamshinda yeye kwa hilo. "Imeandikwa" kila mahali " imeandikwa" kwahiyo alimshinda shetani kwakutumia Mungu. ***(Matayo 4:1-11)***. [7]

Silaha zetu Yesu Kristo ndio Bwana mashetani yote yanafunga breki zao yanapoona hilo. Yanapoona silaha zote za Mungu, ubatizo wa kweli wa Roho Mtakatifu, ukionekana ukija moja kwa moja kutoka kiti cha enzi cha Mungu,ikiwa imevalishwa katika silaha zote kamilifu za kufufuka kwake…Amen [8].

Enyi Wakristo hebu na tuvae silaha zote za Mungu, hebu na tufanye vyote tujuavyo kufanya kumtumikia yeye, kumpenda yeye, na kusubiri ule wakati mkuu. [9]

Silaha za Mungu zinakuja ndani ile nguvu za Mungu zilizofichika Rohoni ambazo akili haziwezi kuona hizo hata kidogo. ***(2 Wakorintho 4:7-10)*** Yesu kamwe hajasema, " Je uliona hiyo" Yeye alisema " unaiamini hiyo" Amen [10].

Kama iko pamoja na neno iko hivyo.Sasa tunajuwa tunavitu vinavyoigiza kila mahali hiyo ni kweli. Ni vita lazima umjue adui yako na inabidi ujue silaha zako. Silaha zako ni neno la Mungu. Adui yako ni kitu chochote kitakachohoji kinyume na hilo. Ndugu silaha zote za Mungu ni ubatizo wa Roho Mtakatifu ukiwa pamoja na neno nyuma yake na kama mtu yoyote akisema wana Roho Mtakatifu na wanapinga neno moja la hili hapo sasa huyo siyo Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu aliandika hii biblia naye alisema "Yoyote atakayeondoa lolote katika hili, au atakayeongeza chochote katika hili sehemu yake itaondolewa katika kitabu cha uzima
***(Ufunuo 22:18-19)*** Roho Mtakatifu anatambua neno peke yake kwasababu hilo ni neno lake na hawezi akaenda kinyume na neno lake. Inabidi alishike neno Lake. Amen [11]

Ni mambo mangapi ambayo ilibidi ayasikilize? Moja tu yeye alinyanganywa silaha palepale ***(Mwanzo 3:1-3)*** shetani alifanya nini aliingia akilini mwake moja kwa moja mpaka kwenye Roho yake, na pale alipotoshwa. Je hiyo ni kweli? A`lipotoka dakika ileile aliponyan'ganywa silaha. Pale aliposhindwa kuamini ***NENO*** la Mungu. Hiyo ni sahihi, sasa hapa tunaona mbinu zake. Sasa kabla vita vyovyote havijaanza jambo la kwanza wanachagua mahali pakukutania au

mahali vita itabidi ipigane mahali palipochaguliwa katika ile vita ya kwanza viliwekwa mahali ambapo siyo ardhi ya mtu yoyote na sehemu ambazo walipigania ilibidi iwe ni sehemu iliyochaguliwa na mahali hapo panaeneo la makubaliano kwamba siyo ardhi ya mtu yoyote na hapo sasa wanaanza kupigana na hapo mahali pa kupigania huanza katika akili ya mwanadamu. Hapo ndipo vita vinapoanza akili ya mwanadamu ndiyo iliyochaguliwa kwaajili ya kuanzia vita mahali ambapo vinaanzia na hiyo ni kwasababu maamuzi yanafanyika kupitia akili ya Mtu. Maamuzi yanafanyika akilini, kichwani hapo ndipo shetani anakutana na wewe. Hapo sasa shetani anaanza katika mahali pa muhimu kumfanya Roho ya mtu ione shaka neno la Mungu. Na Mungu anaanza katika sehemu ya muhimu, ili kuweka neno lake katika Roho. Upo hapo. Hilo ndilo linalofanya hivyo sasa, hapo ndipo vita vinaanza , hapo kwenye akili zake, iwe unataka…

Sasa Kumbuka hiyo siyo habari ya Ukristo wa usayansi kuweka akili kwenye kitu hilo halina……. Ile akili inaukubali uhai ambalo ni neno la Mungu ***( Yohana 6:3)*** na hapo linaleta uzima. Siyo wazo lako tu linalofanya hivyo lakini ni lile neno la Mungu, linaletwa katika mkondo wa mawazo yako. Unaona? Siyo lile wazo kama vile wakristo wasayansi wanavyolifanya akili kwenye kitu hilo siyo hivyo. Lakini akili yako inakubali hilo na inalinasa hilo akili yako inatawaliwa na nini? Roho yako na Roho yako inanasa lile neno la Mungu na hicho kitu kilicho na uhai ndani yake. Kina leta uhai kwako oh! Ndugu hyilo linapofanyika uzima unapokuja chini pale katika mkondo ndani yako, neno la Mungu linadhihirishwa kwako. "Mkikaa ndani yangu na maneno yangu ndani yenu hapo sasa omba utakalo litafanyika kwako" ***(Yohana 15:7)*** Hilo linafanya nini kutoka katikati ya Moyo, ambayo ndiyo nafsi kutoka hapo kuna toka kule kuhudumia kila mkondo . Tatizo lililopo ni tunasimama hapa na mashaka mengi, na kujaribu kuchukuwa kilichopo nje kule. Inabidi uache hilo na uje hapa chini katika mkondo wa neno la kweli la Mungu na hapo sasa linatoka lenyewe tu automatiki ni kile kilichopo ndani ndicho kinachohesabika. Sasa unasema "Mimi siibi. Mimi sinywi. Mimi sifanyi mambo haya" hilo halihusiani na hicho unaona ni kule ndani haijalishi uu mzuri kiasi gani umuadilifu kiasi gani, mkweli kiasi gani hayo mambo yanaheshimiwa lakini Yesu alisema " Mpaka mtu awe amezaliwa mara ya pili. ***(Yohana 3:3-5)*** Unaona lazima kuwe na kitu kilichotokea ndani pale. Kama hakuna hicho kinakuwa ni kitu bandia cha kuwekwa pale. Lakini ndani ya moyo wako unatamani kufanya hilo kwa vyovyote haiwezi kuwa kitu bandia lazima iwe kitu halisi.

Na kuna sehemu moja tu ambayo hilo linaweza likaja kwako na hiyo ni ule uhuru wa kuchaguwa ambao unakuja katika nafsi ya Mtu kwa mawazo yako " kadri mtu anavyowaza moyoni mwake ndivyo alivyo ***(Methali 23:7)*** Kama ukiwaambia mlima huu ng'oka, na usione shaka moyoni mwako, lakini ukiamini kile ulichokisema kwamba kinatokea, unaweza ukakipata kile ulichokisema ***(Malko 11:23)*** un alipata hilo? Tuko hapo unaona huo uwanja wa mapambano.

Inabidi kikubalike na mawazo yako halafu kiaminike moyoni mwako. Hapo sasa neno la Mungu linakuwa halisi, halafu kila hisi ya Roho na mwili vinakuwa vimejazwa na Roho Mtakatifu. Sasa hisi yako ya Mungu, ufahamu wa Mungu kila kitu kilicho cha kimungu kinatiririka kupitia wewe, hakuna shaka mahali popote. Hakuna kitu kinachoweza kuinuka juu ya hilo. Lakini kama huo mkondo umesafishwa na kutakaswa na umejazwa huko ndani na Roho Mtakatifu, hilo haliji tena kwenye hata kwenye kumbukumbu haijalishi juu ya miss Jones haijalishi miss Jones kile alichokifanya ni wewe na Mungu pamoja na hakuna mtu mwingine lakini ninyi wawili. Tuko hapo. Hapo ndipo vita vyako vilipo muuwe yeye pale mwanzoni, msimamishe akiwa

amekufa katika njia yake siyo ni kwa muda gani unaweza kufanya vita nae vikaendelea. Ni kuvisimamisha hapo hapo! Kama utakuja na utaendelea kuziweka hizo kumbukumbu na mawazo na kila kitu ukivifikiria hivyo "vyema naweza kushindwa. Inaweza isiwe hivyo" Usifanye hivyo hata kidogo tupa pembeni kila kitu na ufungue mkondo na useme "Mungu neno lako milele ni kweli, nalo ni kwaajili ya mimi. Kama kanisa lote la wakristo likishindwa, kama dunia yote ikishindwa lakini mimi siwezi kushindwa kwasababu ninalichukuwa neno lako.
Inabidi ufungue mkondo kwanza inabidi umpate askari, roho mtakatifu akitangulia kwenye mstari wa mbele wa vita, hiyo inahitaji neno la Mungu, Yeye ni neno na anasimama pale, hakuna kinachoenda kusimamisha hilo hakuna. Kila mkondo mwingine umesafishwa vizuri kama tu vile chungu cha kuchemshia cha zamani kikiwa na vitu vyote vimewekwa vizuri. Unaweka moto ndani itaenda kulipua kitu chako hivyo ndiyo tatizo walilo nalo wakristo wengi wamelipuliwa kwasababu hawasafishi hiyo mikondo, hawaendi ndani chini kule ya utu wa ndani lazima usafishe hiyo mawazo, kumbukumbu, hoja, kila kitu weka pembeni na ije kutoka ndani kuja nje ikiwa na neno lisiloghushiwa la Mungu kwamba hiyo ni kweli haijalishi maelfu kumi wafe upande mmoja, leo tutaamini maelfu kumi wafe upande mwingine kesho tutaamini kwamba hilo halina chochote cha kufanya na mimi. Mimi ndiye binafsi ndiye ninaye tumainia ndiye ambaye ninaliaamini hilo. Na tunaona kule nyuma kama tungehitaji kufungua mikondo yetu kama tungeweza na kuona.

Tunamuona huyu mmoja na yule mwingine na yule mmoja na yule mwingine tena maelfu yao wakishuhudia. Lakini shetani bado atakuja hapa kama ataweza kuja pale ataweza kulifanya jeshi lako ling'olewe hapo hapo. Kama unahisi zako unaona, huonja, hujiskia, hunusa, na kusikia zote hizo ni nzuri lakini kama hazikubaliani na neno usizisikilize hizo. Sasa mawazo, ufahamu wa kujua jema na baya, kumbukumbu, hoja na upendo vyote hayo ni sahihi kama yanakubaliana na neno. Lakini kama upendo wako haukubaliani na neno uache huo. Utakuletea mafua haraka sana unaona kama hoja zako hazikubaliani na neno achana nazo hizo au zitupilie mbali. Hiyo ni sawa kama kumbukumbu zako kama mawazo yako,kama ufahamu wako wakujua jema na baya haikubaliani na kile kilichopo ndani kitupe nje.

Una kitu gani hapo?  Una sayari zote , nyota zote katika mtiririko (solar system) Halelluya ni Mungu akiwa amezieweka nyota mahali pake akiziambia ning'inia pale mpaka nitakapokuita . Zinakaa pale hakuna kiwezacho kuisogeza Mungu anapoweza kuimpata mtu mkononi mwake mpaka anazipata hisi zake , ufahamu wake wa kujuwa jema na baya na kila kitu kikiwa kimesafishwa vizuri mpaka vyote vinasimama na Mungu nyuma pale. Katika Roho hakuna shetani Duniani anayeweza kuweka shaka mahali pale. [1]

Kumbuka hatupo pikiniki hapa tuko kwenye uwanja wa mapambano. Watu wengi wanafikiri kwamba wanapokuwa wakristo hicho ndicho tu wanahitaji kufanya , wanafikiri hilo linamaliza hilo siku zote ilimradi ni wakristo na kila kitakuja kirahisi kamwe usiweke hicho akilini mwako. Nimekuwa m kristo ili nipigane vita vizuri vya imani ***(2Timotheo 4:7-8)***

Nimekuwa mkristo ili kuingia kwenye mstari wa mapambano. Sisi ni askari wa kikristo inabidi tufundishwe na kulelewa na kujuwa mbinu zote za shetani, kujuwa namna ya kujilinda, kujua namna ya kupigana ***(2 Wakorintho 10:3-6)*** Tunaweza tukafanya hivyo kadri Roho Mtakatifu anavyoweza kutufunulia hatuwezi kuchukuwa kile ambacho taifa linguine linatuambia sisi

tunapoenda vitani. Lakini tunachukuwa mawazo yetu jinsi Roho Mtakatifu anavyotuongoza sisi na mawazo ambayo anatupa sisi kwasababu yeye ndiye mkuu wa majeshi ya wakristo [12].

Sasa ukiwa ndani ya Kristo haimanishi kwamba wewe uko nje huhusiki na vita. Bado uko vitani. Inabidi uipiganie kila nchi ya ardhi ambayo unasimama katika ardhi hiyo . Kwa hiyo kanani haikuwakilisha mbingu kuu kwasababu bado kuna vita na matatizo na kuuwana lakini iliwakilisha jambo hili inabidi iwe kutembea kwa ukamilifu na hapo ndipo kanisa linaposhindwa leo kule kutembea kwa ukamilifu. Je ulijuwa kwamba tabia yako tu binafsi inaweza ikamfanya mtu mwingine akashindwa kuponjwa ukishindwa kufanya vizuri zambi isiyotubiwa za ninyi waaminio. Inaweza ikasababisha kanisa likashindwa vibaya na katika siku ya hukumu utawajibika kwa kila moja ya hilo wewe unasema " sasa hebu subiri kwa dakika ndugu Branham" Vyema hiyo ni kweli fikiri juu ya hilo. [13].

Nimekuwa nikihubiri kwa miaka name nimekuwa mtu mzima na mtu mzee katika huduma na nimekuwa na vita vingi vigumu sana na pengine nimeshikwa na hali ya hofu na wakati mwingine nimekatwa ndani sana kutokana na mapigano kwasababu fungu langu ambalo bwana amenipa mimi siyo kuhusu watoto na kuwafungishia ndoa vijana na kuwazika waliyo wazee. Lakini ni kushika upanga ukatao kuwili katika mstari wa mbele. Nikienda kinyume na mafundisho ya kipagani na mapepo na nguvu za giza na kupigana kwa kutumia neno la Mungu mpaka nimeona adui ameshindwa mara nyingi nimekatwa au nimeumizwa ndani sana. [14].

**NUKUU ZA KINGEREZA.**

[1*].Vita vikuu vilivyowahi kupigana (62-0311) , aya 52-55, 60-63,326-349,297,64-81,91-95,104,108.*
*[2]. Mungu akijificha katika urahisi (63-04E) Aya 70-73.*
*[3]. Yeye anajali je wewe unajali (63-0721) aya 95.*
*[4] Ushawishi [64-0315] Aya 35*
*[5]Kumuita Yesu kwenye kituko (64-0319) aya 11.*
*[6] Jehova Jire sehemu ya pili (64-0403)aya 270.*
*[7] Kutambulishwa kwa kile kipeo cha Mungu (64-1205)aya 128.*
*[8]. Ukristo unavyopigana na upagani (61-1217) aya 200.*
*[9]. Je Mungu hubadili nia yake ndani ya neno lake. (65-0418E) Aya 14.*
*[10] Vaa silaha zote za Mungu (62-0607) Aya E-73.*
*[11]. Kuchukuwa silaha zote za Mungu (62-0701) aya E-56, E-100.*
*[12]. Kanisa lililodanganywa na dunia (59-0628M) aya 8*
*[13]. Kufanywa wana sehemu ya kwanza (60-0515E) aya 53-54*
*[14] Kusimama kwenye pengo (63-0623M) Aya 54.*

---

Jiwe la kiroho la kujengea na. 12 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, Yamekusanywa na Gerd Rodewald friedenstr. 69 D-75328 Schomberg, Germany Simu (+49) 72357613 Fax: (+49) 72353306

---

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyokusudiwa kimbele imesikia.

(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)

*Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:*

*Charles E. Y. Kanju.*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*